# Misaada ambayo huwezi kutumia ufadhili wa NDIS

Swahili | Kiswahili

## Msaada na hati hii

Unaweza kupata mtu wa kukusaidia:

- kuelewa hati hii
- kupata habari zaidi.

Maelezo ya mawasiliano yapo mwishoni mwa hati hii.

## Kuhusu hati hii

Shirika la Kitaifa la Bima ya Ulemavu (NDIA) liliandika waraka huu.

Tunapotumia neno sisi, maana yake ni NDIA.

Tunatoa Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Ulemavu au NDIS.

Hati hii inahusu usaidizi ambao **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS.

# Ni nini katika hati hii?


Gharama za maisha za kila siku 4

Misaada ambayo haina ushahidi unaotegemea 5

Misaada ambayo inahusu afya 5

Misaada inyohusiana na afya ya akili 6

Usaidizi unaohusiana na ulinzi wa mtoto na usaidizi wa familia 6

Misaada inayohusiana na ukuaji wa utotoni wa mapema 6

Misaada inayohusiana na elimu ya shule 7

Misaada inayohusiana na elimu ya juu na elimu ya ufundi na mafunzo 7

Misaada ambayo inahusiana na ajira 8

Misaada inayohusiana na miundombinu ya makazi na jamii 8

Misaada inayohusiana na usafiri 8

Misaada inayohusiana na haki 9

Misaada inayohusiana na utunzaji wa wazee 9

| | |
|---|---|
| Bidhaa na huduma za haramu | 9 |
| Mapato mabadala | 10 |
| Maelezo zaidi kuhusu hati hii | 11 |
| Pata maelezo zaidi kuhusu NDIA | 11 |
| Pata usaidizi ili kuwasiliana nasi | 11 |

## Gharama za maisha za kila siku

Gharama za maisha za kila siku ni vitu unavyoweza:

- kununua kila siku
- kulipa kila mwezi.

Kuna maeneo 8 ya gharama ya maisha ya kila siku ambayo **huyawezi** kutumia ufadhili wa NDIS.

1. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa gharama za malazi na kaya.

Gharama ya malazi na kaya inamaanisha gharama za mahali unapoishi.

2. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa fedha na malipo.

Fedha na malipo inamaanisha pesa unazompa mtu mwingine.

Kwa mfano, pesa unazotoa kwa kanisa.

3. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa chakula na mboga.
4. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa gharama za mtindo wa maisha.

Kwa mfano, sigara na pombe.

5. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa mavazi na urembo.

Kwa mfano, kukata nywele.

6. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa kusafiri na usafiri.

Kwa mfano, kwenda likizo.

7. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa wanyama wa kipenzi.

8. Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa gharama zinazohusu uzazi na familia.

Gharama zinazohusu uzazi na familia zinamaanisha gharama kukusaidia kupata mtoto.

## Misaada ambayo haina ushahidi unaotegemea

Kutegemeana na ushahidi maana yake ni kwamba kitu kimethibitishwa kuwa chenye ufanisi na manufaa.

Ufanisi unamaanisha kitu kinafanya kazi vizuri.

Manufaa inamaanisha kuwa kitu ni kizuri kwako.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa tiba mbadala.

Tiba mbadala ni pamoja na mambo kama vile:

- tiba ya kioo
- tiba ya kubembeleza
- tiba ya michezo ya kubahatisha
- tiba ya kufundisha
- tiba ya nishati.

## Misaada ambayo inahusu afya

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- matibabu ya tatizo la kiafya ambalo si sehemu ya ulemavu wako
- dawa
- huduma za gari la wagonjwa.

## Misaada inyohusiana na afya ya akili

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- dawa za kutibu tatizo la afya ya akili
- huduma za afya ya akili hospitalini
- matibabu ya matatizo ya madawa ya kulevya na pombe.

## Usaidizi unaohusiana na ulinzi wa mtoto na usaidizi wa familia

Ulinzi wa mtoto unamaanisha kusaidia kumweka mtoto salama.

Msaada wa familia unamaanisha tiba kwa familia.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- programu kwa ajili ya wazazi
- walezi wa watoto wa muda
- ushauri nasaha wa ndoa.

Ushauri nasaha wa ndoa ni pale mtu anapokusaidia matatizo katika ndoa yako.

## Misaada inayohusiana na ukuaji wa utotoni wa mapema

Ukuaji wa utotoni wa mapema unamaanisha jinsi mtoto anavyokua na kujifunza mambo mapya.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa mambo kama vile huduma ya watoto.

## Misaada inayohusiana na elimu ya shule

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- sare za shule
- ada za shule
- vitabu vya shule.

## Misaada inayohusiana na elimu ya juu na elimu ya ufundi na mafunzo

Elimu ya juu maana yake ni elimu inayofanyika baada ya kumaliza shule ya upili. Kwa mfano, chuo kikuu.

Elimu ya ufundi na mafunzo ina maana unajifunza kuhusu kazi.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- ada za chuo kikuu
- huduma kutoka kwa mtu anayefanya kazi katika sehemu inayotoa elimu ya juu.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa usafiri kwenda kwa elimu au mafunzo ukiweza:

- kusafiri peke yako
- kutumia usafiri wa umma.

## Misaada ambayo inahusiana na ajira

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- huduma za ajira kwa walemavu
- mambo unayohitaji kufanya kazi yako
- mabadiliko ili kuboresha ufikiaji wa mahali unapofanyia kazi.

Ufikiaji unamaanisha kuwa kila mtu anaweza kuitumia.

## Misaada inayohusiana na miundombinu ya makazi na jamii

Miundombinu ya jamii inamaanisha vitu ambavyo kila mtu anaweza kutumia. Kwa mfano, mbuga na majengo ya umma.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- nyumba kwa watu wanaohitaji mahali pa kuishi
- huduma kwa watu ambao hawana mahali pa kuishi
- mabadiliko ambayo hufanya iwe rahisi kusogea katika jengo.

## Misaada inayohusiana na usafiri

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa:

- mabasi
- treni
- tramu
- usafiri kwa wanyama kipenzi wa kufuga na wanyama rafiki.

Wanyama rafiki ni wanyama ambao hukusaidia kujisikia utulivu.

## Misaada inayohusiana na haki

Haki ni pale unapotenda uhalifu na lazima uende mahakamani.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa huduma ya kila siku ya mtu aliye chini ya ulinzi. Kwa mfano, mtu aliye gerezani.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa ripoti za kabla ya hukumu kuhusu afya yako ya akili.

Ripoti za kabla ya hukumu inamaanisha kuwa mtaalamu humwambia hakimu kuhusu afya yako ya akili.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa usimamizi na ufuatiliaji.

Usimamizi na ufuatiliaji unamaanisha mtu anahakikisha unafanya jambo sahihi.

## Misaada inayohusiana na utunzaji wa wazee

Utunzaji wa wazee unamaanisha utunzaji unaopokea unapozeeka. Kwa mfano, unapokuwa na umri wa miaka 65 na zaidi.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa huduma za kawaida za utunzaji wa wazee.

## Bidhaa na huduma za haramu

Haramu maana yake ni kitu ambacho hakiruhusiwi.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa kitu ambacho hakiruhusiwi.

Kwa mfano, huwezi kutumia ufadhili wa NDIS kwa dawa haramu.

## Mapato mabadala

Mapato mabadala yanamaanisha pesa unazopata ikiwa:

- huna kazi
- huwezi kufanya kazi.

Wewe **huwezi** kutumia ufadhili wa NDIS kwa mambo kama vile malipo ya mkopo.

## Maelezo zaidi kuhusu hati hii

Kwa habari zaidi kuhusu hati hii, tafadhali wasiliana nasi.

Unaweza kutupigia simu **1800 800 110**

Unaweza kututumia barua pepe **enquiries@ndis.gov.au**

Unaweza kutembelea moja ya ofisi zetu kibinafsi

Unaweza kupata ofisi ya eneo lako kwenye tovuti ya NDIS.
**ndis.gov.au/contact/locations**

## Pata maelezo zaidi kuhusu NDIA

Tembelea tovuti yetu **ndis.gov.au**

Tufuate kwenye chaneli zetu za kijamii

**Facebook, Twitter, Instagram, YouTube, LinkedIn**

## Pata usaidizi ili kuwasiliana nasi

Kwa watu wanaohitaji msaada wa Kiingereza Unaweza kupiga simu kwa

Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS) **131 450**

Kwa watu ambao ni viziwi au vigumu kusikia Unaweza kutumia

Huduma ya Kitaifa ya Kuwasiliana kwa Zamu. **relayservice.gov.au**

Unaweza kutumia hali ya simu ya maandishi (TTY). **1800 555 677**

Unaweza kutumia zamu ya sauti. **1800 555 727**